**JINA………………………………………………………………… NAMBARI……………**
**DARASA…………………………………………………………………TAREHE………………**

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya III
Kidato cha IV
Muda: Saa 2½

# MOKASA II PRE-MOCKS 2019

## *The Kenya Certificate of Secondary Examination*

KISWAHILI
Karatasi ya III
Kidato cha IV

**MAAGIZO**

- Jibu maswali manne pekee
- Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki – Riwaya,Tamthilia, Hadithi fupi au Fasihi Simulizi
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Kila swali lina alama 20
- Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
- Watahiniwa wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na maswali yote yamo

## SEHEMU YA A: USHAIRI

**LAZIMA**

**1**. ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Tunda ni kuliangua, chungwa liloninginia,
Tunda pia kuchumia, mbuga sima yowelea,
Jinginelo lipo?

Tunda kivuno shambani, lima kisha palilia,
Tunda vinono nyumbani, kwa jasho shughulikia
Jinginelo lipo?

Tunda tokeo la kazi, na ujira jipatia,
Tunda matokeo wazi, jitihada jifanyia,
Jinginelo lipo?

Tunda pia ni kizazi, wana hao niliozaa,
Tunda tama ya ulezi, wana wataponifaa,
Jinginelo lipo?

Tunda letu la uhuru, minyororo jikongoa,
Tunda sote kuwa huru, na mazao furahia,
Jinginelo lipo?

Tunda ni wetu uchumi, na chumo kujichumia,
Tunda mwenzangu huchumi, ukaweza kwendelea
Jinginelo lipo?

Tunda bora utu mwema, yako roho kuilisha,
Tunda la roho nasema, mja kumkamilisha,
Jinginelo lipo?

**Maswali**

(a) Shairi hili lina bahari kadha zitaje na ueleze. (alama 4)
(b) Eleza vina na mizani ya ubeti wa sita na saba. (alama 4)
(c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)

(e) Taja maana ya 'tunda' kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
(f) Eleza maana ya maneno haya kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
(i) Kuliangua
(ii) Palilia
(iii) Kujichumia.

**SEHEMU YA B: FASIHI SIMULIZI**

**2**. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

**Sungura alivyokwepa kuliwa na samba**

Wanyama wa pori waliamua siku moja kumtuma mnyama mmoja kila siku alikoishi simba kama chakula. Siku moja ilikuwa zamu ya sungura kwenda huko. Sungura alikuwa mjanja sana. Alipanga mpango mzuri wa kumwangamiza simba.

Alienda alikoishi simba muda mrefu baada ya muda wa chakula wa simba. Alimkuta simba akiwa na hasira kubwa sana.

``Kwa nini umechelewa jinsi hii?`` aliuliza kwa hasira.

'Bwana wee,`` alisema sungura kwa sauti ya upole.

``Nilichelewa kwa sababu simba mwingine alinikimbiza. Nilitaabika sana kabla ya kupata upenyu wa kutoroka.``

``Simba mwingine? Je, katika pori hili?`` aliuliza samba.

``Ndiyo bwana mkubwa. Najua anakoishi. Tuandamane nikakuonyeshe,`` alisema sungura.

Simba alijitayarisha kuandamana na sungura. Sungura aliongoza njia hadi walipofika mahali palipokuwa na kisima kikubwa. Sungura alimgeukia na kusema, ``Anaishi hapa. Tafadhali njoo umuone!``

Simba alisogea ulipokuwa ukingo wa kile kisima. Aliyatupa macho huko na kukiona kivuli chake. Alidhani kuwa huyo alikuwa simba mwingine. Kwa hasira kubwa alifungua kinywa na kunguruma. Alimwona huyo simba mwingine akikenulia meno. Simba hakuweza kusubiri, alijitosa kisimani apambane na simba huyo. Huo ulikuwa mwisho wake. Sungura aliondoka akicheka akifurahi kuwa sasa wanyama hawataliwa tena na simba.

**Maswali**

a) i) Andika aina ya hadithi hii

(Alama 2)

ii) Taja sifa tatu za kutambulisha aina hii ya hadithi

(Alama 3)

iii) Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi kwa jamii

(Alama 3)

b) Kwa kutoa mifano taja aina mbili ya fomyula ya:

(Alama 4)

i) Kuanza hadithi

ii) Kumalizia hadithi

c) Eleza sifa nne za mtambaji bora katika fasihi simulizi

(Alama 4)

d) Tofautisha kati ya vipera viwili vya fasihi simulizi.

i) Mighani na maghani

(Alama 2)

ii) Lakabu na misimu

(Alama 2)

**SEHEMU YA C:**
**RIWAYA: CHOZI LA HERI:ASSUMPTA K.MATEI**

**3**. Maovu yametamalaki katika jamii ya Riwaya ya Chozi la Heri, tetea kauli hii kwa kutolea hoja kumi ( alama 20)

**4**. Auntie Sauna alishikwa na polisi "

a. Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
b. Huku ukitoa mifano, fafanua sifa tatu za msemaji (alama 6)
c. Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hii (alama 2)
d. Ni kwa nini Auntie Sauna alishikwa na polisi? Elezea kikamilifu (alama 8)

**SEHEMU YA D:**
**TAMTHILIA : KIGOGO: PAULINE KEA**

**5**. Ami? Tangu lini ukawa ami yangu? **(ALAMA 20)**

a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama2)

b) Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hili. (alama2)

c) Eleza sifa za Msemaji (alama8)

d) Bainisha maudhui ya nafasi ya mwanamke ukizingatia mhusika huyu. (alama8)

**6**. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika Tamthlia hii. (alama 20)

a) Kinaya
b) Majazi

**SEHEMU YA E: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE**
**HADITHI FUPI: ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA**
**SHIBE INATUMALIZA**

**7.** "Ndugu yangu kula kunatumaliza"
"Kunatumaliza au tunakumaliza"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua maana ya kitamthali katika kauli 'kula tunakumaliza' (alam 10)

(c) Kwa mujibu wa hadithi hii, ni kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (alama 6)

**AU**

**8**. (a) "Mame Bakari"
Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka. (alama 10)

(b) "Masharti ya Kisasa"
"…mapenzi ni mateso,ni utumwa, ni ukandamizaji , ni ushabiki usio na maana."
Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi.(alama 10)

# MOKASA II MUHULA WA PILI 2019

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**KISWAHILI –FASIHI KIDATO CHA NNE:**

**1. SEHEMU YA A: USHAIRI**

(a) Tathlitha – Mishororo mitatu kila ubeti
Kikwamba – neno tunda kurudiwa rudiwa
Msuko – Kibwagizo mizani chache.
Ukara – Vina vya nje vyatiririko – vya ndani vyabadhuabadilika. ( alama 4 )

(b) Vina : Ubeti 6 | Ubeti 7.

| | |
|---|---|
| Ubeti 6 | Ubeti 7. |
| mi, a | ma – sha |
| mi, a | ma, sha |
| po | po |

Mizani :

| | |
|---|---|
| ubeti 6 | Ubeti 7 |
| 8, 8 | 8, 8 |
| 8, 8 | 8, 8 |
| 6 | 8 |

(alama 4)

(c ) Tunda ni kivuno kinachotoka shambani baada ya kulima na kupalilia. Mazao mazuri hupatikana baada ya kushughulika kwa jasho. Je, kuna lingine? (alama 4 )

(d) Balagha (alama 2 )

(e)
- Zao la mti
- Tokeo la kazi
- Kizazi / watoto
- Uhuru
- Uchumi
- Vitu wema
- Kutoa matini

(f) (i) Kutunda
(ii) Kulimia
(iii) Kujitafutia riziki ( alama 3 )

**SEHEMU YA B:**
**FASIHI SIMULIZI**

**2.**
a) i) Ujanja na uongo hujitokeza.

ii) Ushindi hujitokeza
Huwa na ubunifu mkubwa
Hustaajabisha na kuchekesha

iii) – Hutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja.
- Hufunza watu juu ya kutenda wema.
- Huonya juu ya upumbavu.
- Huwaokoa wanaodhulumiwa kwa kutumia uwezo mkubwa wa kiakili wa mhusika.
- Hufunza kuwa katika ulimwengu ulojaa hila na shaka, silaha ya maisha ni maarifa, wema na uadilifu.

Zozote 3 x 1

b) Kuanza hadithi
- Paukwa, pakawa, sahani ya mchele, giza la mwizi...........
- Hapo zamani za kale paliondokea.
- Hadithi ! hadithi! Hadithi njoo........
- Kaondokea, chengangaa, kajenga nyumba kaka, mwanangu mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita......

Zozote 2 x 1

Kumalizia hadithi
- Hadithi inaishia hapo
- Tangu siku hiyo
- Wakaishi raha mustarehe
- Maadili

Zozote 2 x 1

c) - Uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
- Mbunifu – anaweza kubadilisha papo hapo katika usimulizi wake.
- Mcheshi.
- Huigiza/kutumia vitendo/ufaraguzi.
- Hutumia ishara kueleza ujumbe.
- Hushirikisha hadhira.
- Huelewa utamaduni na lugha ya hadhira yake.
- Matumizi mazuri ya jukwaa.
- Uwezo kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v huzuni.
- Uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

Zozote 4 x 1

d) i) Mighani – hadithi za fasihi simulizi zinazosimulia mashujaa au majagina.
Hadithi za kihistoria.
Wahusika hupigania haki ya wanyonge.

1 x 2

Maghani – Aina ya ushairi wa kujigamba ambao hutolewa kwa kalima au maneno badala ya kuimbwa.

1 x 2

ii) Lakabu

-Ni majina ya kupanga, kubandikwa au ya utani ambayo watu hujipa au kupewa kutokanan na sifa au hulka na maumbile.

1 x 2

Misimu

- Maneno yanayozuka na kutumiwa katika mazungumzo na makundi maalum ya watu katika jamii
- Mengine huzuka na kutoweka baada ya muda.
  1 x 2

(a

**SEHEMU YA C: RIWAYA**
**CHOZI LA HERI : ASSUMPTA K.MATEI**

**3.** Katika jamii hii kuna biashara haramu kama ile ya uuzaji wa dawa za kulevya. Dick alipotekwa nyara alilazimika kuuza dawa za kulevya kwa muda wa miaka kumi.

Kuna ukabila. Suala hili la ukabila ilijitokeza kikamilifu wakati kulizuka vita vya baada ya kutawazwa. Majirani waliwageuko wenzao ambao walikuwa wametoka katika kabila au ukoo tofauti na wao.

Kuna mauaji. Watu wengi waliwapoteza wapendwa wao kutokano na migogoro iiyozuka baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya.

Katika jamii hii kuna matumizi ya pombe haramu vijana wa vyuo vikuu wanabugia pombe hii ya sumu inayowafanya wengine kuiaga dunia.

Kuna ukeketaji wa watoto wa kike. Wasichana wa Shule ya msingi wanapashwa tohara. Wasichana wengine wanayapoteza maisha yao huku wengine wakiponea chupuchupu na kuwa hospitalini kwa mfano Tuama anayeitetea mila hii iiyopitwa na wakati aliponea kidogo kuiaga dunia.

Ndoa za mapema. Wasichana wachanga wanalazimishwa waolewe na vizee na kuacha masomo yao.

Kuna na uporaji wa mali ya wengine. Wakati vita vya baada ya kutawazwa kuzuka, watu walionekano kupora maduka ya Kihindi, Kiarabu na hata ya Waafrika wenzao.

Katika jamii hii wanawake huavya mimba. Sauna alipachikwa mimba na babake mlezi. Mamake mzazi alimsaidia kuavya kisha akamwonya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama wa babake.

Kuna baadhi ya wazazi wanaohusiana kimapenzi na watoto wao. Sauna alipachikwa mimba na babake mlezi. Mamake mzazi alimsaidia kuavya kisha akamwonya dhidi ya kumwambja yeyote kuhusu unyama wa babake.

Wanawake wengine katika jamii hii wanawaacha waume zao na familia zao na kwenda kuyaishi maisha yao kwingineko. Mamake Umulkheri aliwaacha na kwenda kuishi mjini. Rejelea mhusika Naomi. (Mwanafunzi aongeze hoja nyingine) .

**4.** Auntie Sauna alishikwa na polisi "

a. Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
Maneno haya yalisemwa na Mwaliko. Alikuwa akiwaambia Umulkheri na Dick. Tendo hili lilitukia katika mkahawa wa Majaliwa walipokutana kisadfa. Hii ni baada ya Mwaliko kumpeleka babake mlezi maeneo yale kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake.

b. Fafanua sifa tatu za msemaji (alama 6)
Msemaji ni mwaliko. Ana sifa zifuatazo:
i. Mwenye maadii mema- Mwaiko alipoleewa na Mwangemi na Neema aliinukia kuwa ghulamu mwenye nidhamu ya hali yajuu akiwaheshimu wazazi na majirani na kuwatii wazazi.
ii. Mwenye shukrani- Mwaliko aliamua kumnunulia babake chakula cha mchana siku yake ya kuzaliwa kwenye hoteli ya Majaliwa
iii. Mwenye bidii- alifanya bidii masomoni hadi kufikia Chuo kikuu Alijisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu. Mwaliko anafanya kazi yake kwa bidii ya mchwa. Zozote 3x2= 6

c. Tamathali (alama2) Kuchanganya ndimi- Auntie

d. Ni kwa nini Auntie Sauna alishikwa na polisi? Elezea kikamilifu (alama 8)
Baada ya Umu kupiga ripoti kwenye kituo cha polisi kuwa nduguze wanuna wamepotea, Polisi walifanya uchunguzi wao na kujua kuwa walitekwa nyara. Aliyetekeleza kitendo hiki ni kijakazi Sauna. Sauna alikuwa akimfanyia biashara Bi. Kangora. Polisi walipojua mahali alikokuwa akijificha Bi. Kangara, walishika njia hadi nyumbani kwake ambako waliwatia mbaroni Bii Kangara na Sauna. Walifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la ukiukaji wa haki za watoto hivyo basi wakafungwa miaka saba gerezani na kazi ngumu.

**SEHEMU YA D**
**TAMTHILIA**

**5. SWALI LA KIGOGO na PAULINE KEA (ALAMA20)**

Ami? Tangu lini ukawa ami yangu?

e) Eleza muktadha wa dondoo. (alama2)
   - ✓ **Maneno haya yanasemwa na Tunu akiwa ofisini mwa Majoka, akimjibu Majoka baada ya kumtaka amsalimu yeye ‘ami’ yake.**

f) Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hili. (alama2)
   - ✓ **Swali balagha – Ami? Tangu liini ukawa ami yangu?**

g) Eleza sifa za Msemaji (alama8)
   - ✓ **Nafasi ya Tunu kama mwanamke.**
   - ✓ **Jasiri – Anamkabili Majoka na kumuambia atakavyo. Hamuogopi hata ingawa anamtisha**

- ✓ **Mwenye msimamo thabiti – Ameamua kuwa hatakubali kuoewa na Ngao Junior na anashikilia msimamo wake liwe liwalo hataki kuyumbishwa na lolote lile.**
- ✓ **Mtetezi wa haki – Anashirikiana na wananchi wengine ili kuhakikisha kuwa soko limefunguliwa. Aidha anahakikisha kuwa kigogo ametlewa mamlakani.**
- ✓ **Hakati tama – Hata baada ya kulemeazwa, anaendelea na harakati za ukombozi. Haogopi hata akitembea kwa kiti cha magurudumu.**

h) Bainisha maudhui ya nafasi ya mwanamke ukizingatia mhusika huyu. (alama8)

- ✓ **Tunu ametumiwa na mwandishi ili kupitisha maudhui muhimu. Amedhihirisha nafasi nzuri ya wanawake katika jamii. Kwanza, amedhihirisha kuwa, wanawake ni watu ambao wanaweza kusimama kidete ili kutetea maslahi ya wanajamii kwa jumla.**
- ✓ **Aidha, amedhihirisha kuwa wanawake pia wanaweza kuwania nafasi za uongozi na kuwaongoza watu kikamilifu bila woga na kwa ujasiri kupitia kwa Tunu pia, tumeweza kufahamu kuwa utamaduni wa kuchaguliwa mume umepita na wakati.**
- ✓ **Amembainishia wazi kuwa hawezi kuolewa na Ngao Junior liwe liwalo.**
- ✓ **Halikadhalika, kupitia kwa Tunu tumeona kuwa wanawake sio watu wa kukatizwa tama na waume.**
- ✓ **Vilevile amebainisha kuwa, japo wanawake wanahusika katika siasa, bado hawatayasahau majukumu yao ya kike na pia hawatapotoka kimaadili. Anakuwa mshirika wa karibu wa Sudi lakini hajihusishi naye visivyo.**

**6**

**a)Matumizi ya kinaya**

Ni kinyume cha matarajio kumaanisha kinyume cha yale yasemwayo

- Walimu wanaongezewa mishahara lakini kodi inapandishwa.
- Ni kinaya kwa Majoka kutangaza sherehe ya mwezi mzimakusherehekea ufanisi wa Sagamoyo ilhali hakuna maendeleo.
- N
  i kinaya kwa uongozi kumruhusu mamapima kuuza pombe haramu ilihali sheria inakataza.
- Ni kinaya kuwepo kwa kampuni inayozalisha sumu ya nyoka inayowaua raia wake k.m Ngao junior.
- Ni kinaya kwa wanasagamoyo wanaofanya biashara ndogondogo wanatozwa. ushuru wa juu na hata hongo ilihali hawapewi huduma yoyote.
- B
  oza anamsifia mkewe ilihali mkewe anamsaliti kwa kushiriki ngono nje yandoa.

**(b) Majazi**

Ni mbinu ya kuwapa wahusika au mahali majina kulingana na sifa zake

**MAJOKA-** Ni wingi wa neno joka. Kwa kawaida, joka huwa na sumu inayoua

- Utawala na matendo ya majoka ni kama sumu/ nyoka kwa raia,
- k.m wandamanaji wanauawa, kwa mfano baadhi ya raia wanakufakutokana na sumu ya nyoka.

**TUNU** -Hii ni tuzo hidaya au zawadi.

-Tunu ni kama zawadi kwa wanasagamoyo kwani anatia bidii katika kutetea haki zao, Wananchi wanamtaka kuwania uongozi wa sagamoyo ili awe kiongozi wao

**SUDI**~ Sudi inamaanisha bahati.

-Ana bahati ya kuwa na mke mzuri , mwenye bidii na mtetezi wa haki, ama ana bahati ya kuwa na kipaji cha uchongaji wa vinyago vizuri akilinganishwa na wachongaji wengine.

**MAMAPIMA** -Ni mama ambaye anafanya kazi ya kuuza pombe hivyo jina lake limetokana na kuwapimia walevi pombe.

**SAGAMOYO-**Kuusaga moyo ni kuumiza moyo au kupitia katika hali ngumu ya mateso makubwa yanayosaga mioyo yao.

**NGURUMO** -Ni sauti ya kutisha.Matendo ya ngurumo ni ya kutisha kwa mfano kulewa kupita kiasi, matusi, na hata kushiriki katika kumvunja Tunu mguu.

**CHAPAKAZI-**Jina hili linamaanisha bidii,

Soko la Chapakazi ni mahali ambapo wachochole huchapa kazi kwa bidii na kujitafutia riziki yao.

**HUSDA** - Linaashiria au kurejelea neno husuda kwa maana ya kuonea gere. k.m ana husuda dhidi ya Ashua kwa kudhania kuwa anamchukua mumewe kimapenzi . Aidha mumewe anamtaja kama chui katika ngozi ya kondoo.

**SITI-** Ni jina la heshirna la mwanamke,Siti ni binti wa heshima anayetaka haki itendeke katika Sagamoyo ndipo anashirikiana na wanaharakati wengine kuleta heshima ya Sagamoyo.

**PENDO**-Ni mwana wa Sudi na Ashua wazazi wake wanampenda kwani ni matokeo ya pendo la wazazi wake.

**KENGA** - Maana yake ni kudanganya au kulaghai hivyo Kenga anampa Majoka ushauri usiokuwa wa kweli unaompotosha hatimaye.

**SEHEMU YA E**

**<u>SEHEMU TUMBO LISILOSHIBA</u>**

**MWONGOZO WA SHIBE INATUMALIZA**

**7**.a)

- Kauli ya kwanza ni ya mbura
- Kauli ya a pili ni ya sasa.
- Walikuwa nyumbani kwa Mzee Mambo
- Mzee Mambo alikuwa ameandaa hafla ya kusherekea mtoto wake kusajiliwa kwenye shule ya nasari na wa pili meno yalikuwa yamepasua ufizi.
- Wanasema haya baada ya kula sana kwenye sherehe hiyo. **4 x 1 = 4**

b)

- Mzee Mambo kuwa waziri kivuli wa wizara zote – anapokea mshahara lakini hana kazi yoyote.
- Wafanyikazi ni watepetevu-wanafika kazini lakini hafanyi lolote pale kazini.
- Vyeo vya mzee Mmambo vinampa fursa ya kupakuwa mshahara (yeye anachota tu hapewi) uk 37.
- Mzee mambo kuandaa sherehe kubwa ambayo inaangaziwa na vyombo vya habari.
- Wizara moja inaendeshwa na mawaziri wawili – Sasa na Mbura wanadai kuwa wao ni mawaziri wa wizara ya Mipango na mipangilio.
- Sasa na Mbura kuendesha wizara kwa namna ya kujifaidi. Wanasema wizara inawaendesha hasa. Uk 37.
- Magari ya serikali kutumiwa vibaya kwenye sherehe ya Mzee Mambo kuleta jamaa zake, kuleta sherehe havipikwi hapo bali vinaagizwa kwa mali ya umma. Uk 39.
- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wizi wa mali ya uuma.
- Maelezo ya jinsi Sasa na Mbra wanafakamia chakula upsei yanatupa taswira ya jinsi wenye uwezo wanapapia mali ya umma bila kuona haya.
- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wiziz wa mali ya umma.
- Matajiri hawajali lawama kutokana na wizi wao wa mali ya umma.
- DJ kwenue sherehe ya Mzee Mamabo hajali lawama kwa kulipwa mabilioni ya pea kutoka kwenye hazina ya umma.
- DJ ana duka la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kubwa ya dawa za serikali.
- DJ na wenzake wanapaata huduma za kimsingi kama vile maji ya umeme huku raia wakiumia. **(Hoja zozote 10 x 1=10)**

c)

- Magonjwa yanayosababishwa na kula lishe isiyobora mfano sukari, presha, saratani, obesti n.k
- Kuna mauaji- watu wanauana kwa kutumia silaha za maangamizi kama vile risasi na mabomu au hata kunyongana kutokana na unyakuzi wa mali ya umma.
- Kuna hai ya kuuna kifikira na kimawazo.
- Uhalifu wa kunyang'anyana mali.
- Kutovukwa na utu/ukosefu wa heshima.
- Kutojirudi kutokana na makosa wafanyayo/kukosa kukiri na kuomba msamaha watendapo maovu.
- Kuhalalisha wizi/unyakuzi – inasemwa kuwa aliyepewa hapokonyeki (ubinafsi)

**8**. a)

- Tukio la kubakwa linampotesea fahamu na anaaibika sana anapozinduka na kujipata akiwa uchi uk 47

- Mwanamke kujeruhiwa – Baada ya Sara kubakwa na janadume lile, anaharibiwa na kuvuja damu.
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake.
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa.
- Masomo yake yanakatizwa – mwalimu mkuu alimkabidhii Sara barua ya kumfukuza shuleni (uk 49)
- Mwalimu mkuu hamsikilizi wala kumhurumia – badala yake aliongoza kumkejeli na kumweleza ile haikuwa shuke ya wazazi bali wa wasichana. Anasema hawafundishi wanawake hapo.
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara anaingiwa na mawazo mengi jinsi atakvyoukabili ule ujauzito. Anafikiria hata kuitoa ile mimba, kuhama kwao na hata kujiua.
- Mwanamke katika umri mdogo anabebeshwa mimba jinsi Sara alivyofanysihwa. Mzigo huo ungekuwa na changamoto nyingi kutokana na umri wake mdogo.
- Kuishi adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.
- Kuogopa kutoa taarifa ya kubakwa kwa wazazi kwa sababu wazazi hawangemwamini.
- Kuishi maisha ya kimaskini – msimulizi anaeleza kuwa Sara angekuniwakunjiwa matambatra yake na kuruishiwa nje.
- Kila mara mwanamke anapobakwa, anayelaumiwa ni mwanamke na hata huonwa kama shetani. Uk 48 **(hoja 10 x 1 = 10)**

b)

Mtahiniwa azingatie masharati ambayo mwanamume anafaa ayazingatie pamoja na athari zake katika maisha y andoa.)

- Dadi ndiye mchuma riziki-yeye ni muuza samaki na apatacho kinatumiwa kuilisha jamaa yake. Pesa za mkewe ni za kununua fasheni mpya mpya na mapambo.
- Dadi anasaidia kazi za nyumbani lakini mkewe Kidawa hatosheki na hayo.
- Kidawa hakubali kuwa mwanamume kazi ni za nje si za ndani na kuwa Dadi kufanya kazi za ndani ni hisani tu. Uk 60.
- Dadi analazimika kushika shughuli za upishi kama vile kukuna nazi na kutia mboga tui.
- Dadi anaosha nyumba, kufagia, kufua na hata kupiga nguo pasi.
- Wanandoa kujiwekea masharti ya uzazi. Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu kutokana na athari za usasa.
- Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa za kuwauzia wateja. Kila mara mkewe anapofanya hivyo, anaumia sana. Anaiona hiyo kama fursa ya mkewe kuhusiana na wanaume wengine . Uk 61.
- Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashinda kumweleza.
- Licha ya kuwa Dadi aliona ugumu wa kuzingatia masharti aliyowekewa na mkewe, hangeyavunja. Angefanya hivyo ndoa yao ingevunjika na huko kungekuwa ni kumvunja yeye pia.

- Dadi kushuku mkewe ana uhusiano wa kimapenzi na mwalimu mkuu.  Hali hiyo inampa wasiwasi sana hata anashindwa kula.
- Kila mara Dadi alitarajiwa kuwa baada ya kula angeviondoa vyombo mezani na hata kuvisafisha.

Dadi anapoamua kuzua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu akiwa amepanda apipu na anaagnuka na kuumia vibaya sana jambo linalomshutua sana mkewe pamoja na mwalimu mkuu